Kuwa tayari

Fahamu haki na wajibu wako kama mteja wa Bayport

your future now

BAYPORT
FINANCIAL SERVICES

UTANGULIZI

Sisi kama watoa huduma za kifedha,Bayport imefungamana na sheria na kanuni. Kama biashara inayoheshimu na kupenda wateja wake, tuna kanini mbalimbali za ndani ambazo zinawaelekeza wafanyakazi wote namna ya kuhudumia wateja wetu.

Kwa sababu hizi, wewe kama mteja wetu utakutana na taratibu na nyaraka mbalimbali unaposhughulika na Bayport.

Dhumuni la kitabu hiki ni kukusaidia kuelewa maana ya kanuni zetu kwako. Haki zako ni zipi? Wajibu wako ni nini? Nini utarajie/usitarajie kutoka Bayport? Majibu ya maswali yote yapo hapa

Tunatumaini maelekezo haya yatakurahisishia wewe kufanya biashara nasi

KILA MTU NI SAWA

Hapa Bayport tunawatendea wafanyakazi na wateja wetu wote kwa heshima na usawa

Hairuhusiwi mtu yeyote anayefanya kazi Bayport kukunyanyapaa kwa sababu ya

- Rangi
- Dini
- Jinsia
- Umri
- Utaifa au kabila
- Ulemavu
- Hali ya mahusiano
- Hadhi ya kijeshi

Endapo utahisi umtendwa kinyume na haki ,wasiliana na timu yetu ya huduma kwa wateja mara moja:

Huduma kwa wateja:

0800 782 700

UNAPOSHUGHULIKA NA MAAFISA MAUZO WETU

Maafisa wa mauzo wa Bayport ni wenye ari na kazi yao. Tarajia yafuatayo kutoka kwao

AFISA MAUZO ANAPASWA:

- Kufika kwa wakati kwenye miadi yao
- Kuwa nadhifu
- Kukuhudumia kwa uaminifu na heshima.
- Kuwa na kitambulisho kinachomuidhinisha yeye kama wakala halali wa mauzo wa Bayport

AFISA MAUZO HAPASWI:

- Kufika ofisini au nyumbani kwako bila idhini yako
- Kula au kunywa mbelel yako.
- Kukutana na wewe akiwa ametumia kilevi chochote
- Kukudhalilisha
- Kuchukua fedha kutoka kwako.
- Kukukopesha fedha au kukukopa fedha yeye binafsi
- Kutoa mapendekezo kuhusu mambo yako binafsi ya kifedha

Bayport ina sheria madhubuti zinazosimamia mchakato mzima tunaoufuata wakatiwateja anapoomba mkopo

KWA MUJIBU WA SHERIA, AFISA MAUZO HAPASWI:

- Kukaa na kitambulisho asilia au kadi ya benki
- Kutoa taarifa zako kwa mtu mwingine
- Kukushawishi wewe kuchukua mkopo ambao hautaumudu
- Kupokea zawadi za gharama kutoka kwako
- Kuweka saini kwenye nyaraka zozote kwa niaba yako
- Kukutaka uweke saini kwenye nyaraka tupu
- Kukubali nyaraka batili kutoka kwako

MAAFISA MAUZO WETU WANATAKIWA

- Kukupa nakala ya fomu ya maombi ya mkopo
- Kukuelezea vigezo na masharti ya mkopo
- Kukuelezea faida za bima ya Maisha ya mkopo
- Kukagua nakala ya kitambulishi kulingana na kitambilisho asilia.
- Kukupa taarifa juu ya hali ya ombi la mkopo wako
- Kukuelezea mchakato wa mkopo wako kabla ya kuwasilisha ombi lako
- Kuomba rufaa ya mtu unayemjua ambaye anaweza kuwa na uhitaji wa mkopo.

Endapo hautafurahishwa na namna afisa mikopo atakuhidumia, tafadhali toa taarifa haraka.

Huduma kwa wateja:

0800 782 700

UNAPOSHUGHULIKA NA IDARA YETU YA UKUSANYAJI

Kuna wakati wateja wanashindwa kulipa madeni yao na Bayport inabidi kutumia huduma za maafisa ukusanyaji. Tunategemea maafisa ukusanyaji wetu kuwasiliana na wateja kwa heshima

MAAFISA UKUSANYAJI HAWAPASWI

- Kukuogopesha,kukutisha au kukudhalilisha
- Kukutishia kukuripoti kwa mwajiri wako
- Kujadili hali yako na mtu mwingine yeyote kama ndugu,marafiki au mwajiri wako
- Kufanya jambo lolote litakalohatarisha kazi yako
- Kukusanya au kudai kiasi zaidi ya kile unachodaiwa

MAAFISA UKUSANYAJI WANAPASWA:

- Kutenda kwa weledi
- Kuchukulia taarifa zako kama siri
- Kuheshimu haki zako za kibinadamu
- Kutumia njia zilizoidhinishwa na Bayport pamoja na mfumo wa sheria wa Tanzania.
- Kukuambia salio la akaunti yako na kwanini unadaiwa na Bayport.

Endapo hautafurahishwa na namna ukusanyaji atakuhidumia, tafadhali toa taarifa haraka iwezekanavyo:

Huduma kwa wateja:

0800 782 700

UNAPOCHUKIUA MKOPO BAYPORT

Vigezo na masharti vinavyoorodheshwa kwenye fomu ya maombi vinaweza kukupa wasiwasi. Hakikisha unamuuliza afisa mauzo wa Bayport na akuelezee vizuri. Ili kukusaidia kuelewa vigezo hivyo na masharti vizuri, ufuatao ni muhtasari.

UNATAKIWA:

- Kuhakikisha taarifa zote unazojaza kwenye fomu ni sahihi
- Soma fomu, au muombe mtu akusomee kwa usahihi, kabla ya kuweka sahihi yako.
- Ijulishe Bayport endapo kuna mabadiliko yoyote ya akaunti yako au mwajiri.

KWA KUWEKA SAHIHI YAKO KWENYE FOMU, UNAIPA BAYPORT RUHUSA:

- Kuwasiliana na mtu yoyoye, ikiwemo benki husika akaunti yako ilipo, mwajiri wako au ofisi za mikopo, kuhakikisha kama taarifa ulizotoa ni sahihi.
- Kutoa taarifa zako zilizopo kwenye fomu kwa ofisi zote za mikopo.
- Kufanya makatao ya mkopo kutoka kwenye akaunti yako au mshahara wako. Unaweza kughairisha agizo la kulipa kwenye akaunti yako ya benki, lakini unapaswa kutoa taarifa kwa Bayport siku 30 kabla. Kumbuka bado una jukumu la kulipa mkopo wako.
- Kuripoti udanganyifu wowote utakaofanya kwa polisi/Takukuru au shirika lolote la kupambana na uhalifu
- Badilisha tarehe kumaliza mkopo endapo itatokea kuna malipo yatakosekana.
- Kuitisha makubaliano ya mkopo wako na kuomba pesa zote zilipwe kwasababu ya kukosekana kwa malipo.
- Kutuma taarifa zaki kwenda huduma nyingine za Bayport,hata kama umemaliza kulipa mkopo

UNA HAKI YA:

- **Kuelewa kikamilifu kile ambacho unasaini.** Afisa mauzo anapaswa kukuelezea makubaliano ya mkopo mpaka utakaporidhika.
- **Endapo utabadilisha mawazo yako.**Ndani ya siku 10 baada ya kuweka saini unaweza kufuta makubaliano ya mkopo bila kulipa fidia yoyote. Utatarajiwa kurejesha kiasi chochote cha pesa ulichoingiziwa hapo awali.
- **Maliza mkopo wako kabla ya muda.** Tambua Bayport itakutoza ada ya kulipa deni kabla ya wakati.
- Kama haujaridhishwa na huduma za Bayport wasilisha malalamiko yako katika Tume ya Haki ya Ushindani (FCC) na Benki Kuu ya Tanzania

Kumbuka: Makubaliano ya mkopo yanabadilishwa kwa njia uya manndishi tu, na ni endapo wewe na Bayport mmekubalinana

Rejesho lako la mkopo la kila mwezi
=Mtaji + Riba + Ada ya Usimamizi + Bima ya Maisha ya Mkopo

Ikiwa una wasiwasi juu ya jinsi ombi lako la mkopo lilivyoshughulikiwa, au unataka kufungua malalamiko,Tafadhali wasiliana na Bayport mara moja:

Huduma kwa wateja:

0800 782 700

UNAPOTOA BIMA

Unapochukua mkopo wa Bayport, moja kwa moja unahitaji bima.

Bima ya Maisha ya mkopo wa Bayport inahakikisha kuwa deni lote linalobaki linalipwa kwa niaba yako endapo utapata ulemavu wa Maisha,utapoteza maisha au ukipata ugonjwa kama kansa ikiwa utafutwa kazi au kupata ulemavu wa muda, kiwango cha juu cha malipo ya bima ni awamu sita za rejesho.

Malipo yako ya bima yatakatwa pamoja na rejesho lako la kila mwezi.

ENDAPO KUNA MABADILIKO YOYOTE KWENYE MKOPO WAKO, UNAWEZA KUHITAJI:

- Kulipa mkopo wako kwa muda mrefu zaidi
- Kupunguza au kuongeza kiasi cha rejesho la kila mwezi.
- Kulipa mkopo haraka

Yote haya yanaitwa mabadiliko ya mkopo.

UNAPOOOMBA KWA MAANDISHI MABADILIKOYA MKOPO, TARAJIA

- Afisa wa mauzo wa Bayport Bayport kukuomba nyaraka ya malipo ya mshahara ya hivi karibuni.
- Afisa wa mauzo atakabidhi maombi yako kwa Afisa Mkuu wa mikopo.
- Afisa Mkuu wa mikopo atapitia ombi lako kisha ataidhinisha au kukataa
- Kujulishwa kuhusu maamuzi ya Afisa Mkuu wa mikopo.
- Kuelezewa masharti mapya ya mkopo
- Bayport itafanya mabadiliko ya mkopo wako mara tu utakapokubaliana na masharti mapya ya mkataba.

Endapo hautaridhishwa na mchakato wa mabadiliko ya mkopo wako, Tafadhali wasilisha malalamiko yako haraka iwezekanavyo.

Huduma kwa wateja:

0800 782 700

HEAD OFFICE CONTACT DETAILS

Bayport Financial Services Tanzania
3rd floor Al Dua Towers
3/12 Regency Estate, Morocco Junction
New Bagamoyo Road
P.O. Box 71967
Dar es salaam Tanzania

Customer careline: 0800 782 700
www.kopabayport.co.tz

your future now

BAYPORT
FINANCIAL SERVICES